



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

Yah: **MAFUNZO YA UTARAJALI**

Baraza la Uuguzi na Ukunga ni mamlaka ya Kisheria iliyoanzishwa kwa lengo la kusimamia Wataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga ili kuulinda umma dhidi ya huduma zinazotolewa na Wauguzi na Wakunga nchini. Baraza linafanya kazi chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 na Kanuni zake.

Ofisi ya Msajili inapenda kuwataarifu Wauguzi na Wakunga Wahitimu wa Shahada za kwanza za Uuguzi na Ukunga wanaotarajia kujiunga na Mafunzo ya Utarajali kuanzia tarehe 01.04.2023 kuwa dirisha la maombi kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Baraza (www.tnmc.go.tz) litafunguliwa kuanzia tarehe **20.03.2023** hadi tarehe **23.03.2023**

Wahitimu wenye sifa mnatakiwa kuandaa nyaraka zifuatazo kwa ajili ya kukamilisha maombi na kuchagua Vituo pamoja na kuandaliwa Vyeti vya Usajili wa Awali (Provisional Registration Certificates);

- i) Nakala ya Cheti cha kuzaliwa
- ii) Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA)
- iii) Nakala za Vyeti vya elimu ya Sekondari (O-level na A-level)
- iv) Nakala za Vyeti vya Taaluma na Leseni hai (kwa waliotoka kazini)
- v) *Passport size* yenye ukubwa wa **35x35mm**, **back ground ya light blue**

Baada ya kukamilisha taratibu za maombi Watarajali wanatakiwa kufika katika Vituo vya Mafunzo walivyopangiwa kuanzia tarehe **01/04/2023**. Mwisho wa kupokelewa ni tarehe **05/04/2023**.

Kwa ufafanuzi ziada wasiliana kwa namba zifuatazo: **+255 758 589 706**, **+255 628 583 890** na **+255 787 951 966**.

ANGALIZO: Mtarajali yeyote atakayeona hawezi kufanya Mafunzo katika Vituo vilivyopo aahirishe mpaka atakapopata Kituo kinachomfaa.

Nawatakia utekelezaji mwema

Imetolewa na:


Agnes Mtawa

MSAJILI

10. 03. 2023